

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Hamsini na Saba – Tarehe 30 Juni, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Saba, leo ni Kikao cha Hamsini na Saba. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki. Mheshimiwa Nyongo.

Na. 468

Mikopo kwa Walimu Kwa Ajili ya Ujenzi wa Nyumba

MHE. STANSLAUS H. NYONGO aliuliza:-

Walimu Wilayani Maswa wana uhaba wa nyumba za kuishi; pamoja na juhudini za wananchi kujenga nyumba za walimu wa shule za msingi na sekondari lakini walimu hao bado wanahitaji kujenga nyumba zao wenye wewe za kudumu.

Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu maalum wa kutoa mikopo kwa walimu hao ili wajenge nyumba zao binafsi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ina uhitaji wa nyumba za walimu 1,358. Nyumba zilizopo ni 479 na hivyo upungufu ni nyumba 879.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huu Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Maswa ina mpango wa kujenga nyumba 16 katika mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, kati ya nyumba hizo, nyumba nane zitajengwa kwa bajeti ya 2017/2018 (*CDG*) na nyumba nyingine nane zitajengwa kwa kutumia mapato ya ndani y (*own source*) ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa tatizo la upungufu wa nyumba halitaweza kumalizwa na Serikali peke yake, Serikali inawashauri walimu wa Halmashauri ya Maswa na walimu wote nchini wanaohitaji kujenga nyumba zao binafsi kukopa fedha kutoka katika taasisi za fedha zinazokubalika Kisheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inatoa wito kwa walimu nchini kote kujiunga na vyama vyaya kuweka na kukopa (*SACCOS*) ili waweze kukopa kwa riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za binafsi. Pia Serikali inawashauri walimu kutumia mikopo ya nyumba inayotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

SPIKA: Mheshimiwa Ngongo swalii la nyongeza nilikuona.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali langu dogo tu la nyongeza ni kwamba kwa kuwa masharti ya mikopo kwenye mabenki na *SACCOS* nyingi ambazo kwa kweli watu wengi wamekopa na wameshindwa kulipa madeni na yamewasababishia umaskini mkubwa. Je, hamuoni kwamba kuna haja Serikali sasa mkatazama namna nyingine ya kuwapatia walimu hawa mikopo ya masharti nafuu ili waweze kujenga nyumba zao za kudumu? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mna mpango gani wa kuiwezesha Halmashauri ya Maswa kama tulivyoongea siku za nyuma, kwamba Halmashauri na zenyewe ziwe na uwezo au zijengewe uwezo wa kuchukua mikopo ili mikopo hiyo kuititia halmashauri iwasaidie walimu hao kujenga nyumba zao za bei nafuu? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli mikopo mingine inayotokana na taasisi za benki ina changamoto nyingi sana, lakini kwa utaratibu wa sasa wa kuwasaidia wafanyakazi kuna suala la *mortgage financing* ambalo Bunge hili hili lilipitisha sheria humu ndani kuwawezesha watumishi mbalimbali waweze kupata fursa ya mikopo kuititia fedha wanazochangia katika mifuko yao ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika hili naomba niwapongeze *Utumishi Housing* ambao wamefanya kazi kubwa sana katika maeneo mbalimbali hivi sasa. Tunaona wazi kwamba matangazo yao yametoka, sasa naomba tuwaambie watumishi wa Serikali, tutumie dirisha hili vizuri ili tuweze kupata nyumba katika maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuziwezesha Halmashauri mbalimbali hasa Halmashauri ya Maswa, kupata mikopo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inafanya

uwekezaji; kuhusiana na jambo hili mara nyingi sana ofisi yetu huwa inapokea vibali mbalimbali vya kutaka halmashauri kufanya uwekezaji katika eneo fulani. Hata hivyo mara nyingi sana ofisi yetu huwa inapitia haswa yale maombi kuangalia ili jambo likishapitishwa, likapatiwa kibali ambapo lisije likawa mzigo mkubwa sana kwa Halmashauri hiyo kiasi cha kushindwa kujidoresha.

Kwa hiyo, mawazo mazuri yanakaribishwa, na ofisi yetu ina wataalam watafanya *analysis* lile jambo linalofanyika basi Halmashauri hiyo haitawekwa nyuma kuhakikisha kwamba inapewa kibali ili ifanye uwekezaji katika halmashauri yake.

SPIKA: Swali linalofuata Mheshimiwa Rose Kamil Sukum kwa Wizara hiyo hiyo ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Na. 469

Upotevu wa Fedha za Ruzuku ya Chakula Shule za Bweni Wilaya ya Hanang

MHE. ROSE K. SUKUM aliuliza:-

Serikali ina utaratibu wa kutoa fedha kwa ajili ya shule za bweni nchini. Kwa kipindi cha kuanzia tarehe 31/08/2013 hadi 10/02/2014 Halmashauri ya Hanang ilipokea kutoka Serikali Kuu kiasi cha shilingi 508,779,500 kwa ajili ya chakula cha shule za bweni. Taarifa zinaonesha kuwa fedha zilizotumika kununua chakula ni shilingi 225,585,000. Kwa takwimu hizo bakaa ni shilingi 283,194,500 na kwa mujibu wa mkaguzi, bakaa hiyo haionekani kwenye akaunti yoyote ya benki.

(a) Je, fedha hizo zinarudishwa Hazina bila ya uwepo wa nyaraka zozote toka Halmashauri kuonesha muamala unavyofanya kazi?

(b) Je, kama fedha hizo hazikurudishwa Hazina, nani anaweza kuidhinisha matumizi bila ya mpango wake kuitishwa na Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri?

(c) Je, kama fedha zimetumika bila kupangiwa na Kamati halali, ni kwa nini wahuksika bado wanaendelea kuwa ofisini bila ya kufunguliwa mashtaka ya wizi wa kuaminika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA: alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' ilipokea kiasi cha fedha shilingi 508,779,500 kwa ajili ya chakula cha shule za msingi nne za bweni ambazo ni Katesh, Balangdalalu, Bassodesh na Gendabi. Jumla ya shilingi milioni 225.58 zilizopangwa kwenye bajeti zilipelekwa kwenye shule za msingi za bweni kadiri fedha hivyo zilivyopokelewa kutoka Hazina. Kiasi cha shilingi milioni 283.19 zilizosalia hazikurudishwa Hazina badala yake fedha hizo zilibadilishiwa matumizi kwa kuombewa kibali cha kubadilisha matumizi kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kwa barua yenye kumb. Na. HANDC/ED/F.1/12/VOL.IV/198 ya tarehe 10/04/2014 na kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa barua yenye kumb. Na. HAN/ED/F1/12/VOL.IV/205 ya tarehe 01/08/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri baada ya kupokea taarifa ya matumizi ya fedha, iliagiza fedha hizo zirudishwe kuitia mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza shughuli za ununuzi wa vifaa na samani kwa wanafunzi wa shule husika. Ili kutekeleza agizo hilo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016, kiasi cha shilingi 130,000,000 zilipelekwa kwenye akaunti za vijiji vya Gendabi, Bassodesh, Katesh na Balangdalalu kwa ajili ya

kununulia magodoro, vitanda na ukarabati wa mabweni kwa shule za msingi za bweni zilizopo kwenye vijiji hivyo. Aidha, Halmashauri imeagizwa kurejesha fedha zilizobaki kiasi cha shilingi milioni 153.19 ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matumizi ya fedha za halmashauri yasiyoridhisha, ikiwa ni pamoja na matumizi ya fedha hizo, tangu mwezi Aprili, 2016, Mkurugenzi Mtendaji amesimamishwa kazi na mamlaka yake ya nidhamu. Aidha, watumishi wengine wanne akiwemo afisa mipango wilaya, mweka hazina wilaya na wahasibu wawili wamesimamishwa kazi na Baraza la Madiwani ili kupisha uchunguzi.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba unipe fursa niweze kumuelezea Mheshimiwa Waziri alivyodanganywa na waliomjibia maswali haya.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi umeshafanyika Wilaya ya Hanang na uchunguzi huo umefanywa na timu ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara kwa ajili kujua ubadhirifu wa fedha hizo, sio tu fedha za chakula bali ni fedha nyingine pia zipo za shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Spika, nasikitika Mheshimiwa Waziri, nimekuletea *document* hizi za uchunguzi uliofanyika ndani ya ofisi yenu, leo unakuja kujibu kirahisi kiasi hiki ina maana kwamba wewe umedanganywa, haya si majibu yaliyotakiwa. Fedha hizi zimetumika, shilingi milioni 100 unazosisema hizo zimetumika ni fedha za *SEDEP* ziko kwenye uchunguzi hii na nitakukabidhi sasa hivi. Hizi za *SEDEP* zimetumika kwenda kununua magodoro na kadhalika kwenye hayo mabweni. Kwa hiyo ni kosa moja wapo lilitumika la kutumia fedha ambazo hazistahili kutumika.

Mheshimiwa Spika, la pili taarifa ya Mkaguvi wa Ndani imeeleza Aprili 15 zikisema matumizi mabovu ya hizi fedha,

fedha hizi hazikutumiwa na halmashauri zimetumiwa na mtu mmoja au watu wachache ndani ya Halmashauri. Sasa iweje Halmashauri irudishe hizi fedha ili kuweza kulipia deni la mtu ambaye amekula hizo hela? Pia kwa taarifa uliyosema majibu ya Mkurugenzi kwamba amesimamishwa, Mkurugenzi yuko kazini anafanya kazi yuko ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, na hawa watumishi wengine wako Wilaya ya Hanang wanafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba unisaidie, ni kwa nini hawa watumishi hawakuchukuliwa hatua mpaka sasa hivi na taarifa hii iko ofisini kwako?

La pili, kama kweli inatakiwa ithibitike, utatumia hatua gani kuwezesha uchunguzi maalum ufanyike kwa ajili ya kujua ubadhilifu wa fedha za Wilaya ya Hanang? (*Makofii*)

SPIKA: Maswali hayo jinsi yalivyoulizwa yanaonesha uzito wa swali hili na *concern* ya Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wake. Majibu ya maswali haya Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwanza wizi ni wizi hakuna wizi mdogo hakuna wizi mkubwa; wizi ni wizi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Sukum kwamba japokuwa hapa tulikuwa tunaeleza ule mchakato wa zile fedha maalum lakini kilichokuwepo kutokana na *specific questions* ambazo umeuliza ni kwamba inaonekana Halmashauri ya Hanang si hiyo, kuna lidudu likubwa liko katika Halmashauri ya Hanang. Ndiyo maana nimesema wizi ni wizi hauna mjadala.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie, haya yote aliyosema Mheshimiwa Sukum kwamba tutafanyaje, nimesema hapa tumechukua hatua. Kama kuna ubabaishaji wa aina yoyote katika zile hatua tulizochukua naomba nikuhakikishie kwamba *by this week* ambapo leo Ijumaa, *by next week* ofisi yetu itatuma *special investigation team*. Lengo lake kubwa ni kwenda kujiridhisha ni kitu gani kimejificha

ndani ya boksi; kwenda kutatuta tatizo la msingi la fedha ambazo inawezekana zimetumika kinyume cha taratibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, na hili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Sukum; katika jambo hili Serikali ya Awamu ya Tano haitavumilia uzembe wa mtu yoyote wa aina yoyote. Hili naomba niseme kwamba kwa *concern* aliyozungumza Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, tunaiagiza timu yetu ya *investigation and follow up* kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, si kutoka ofisi ya Mkoa, kutoka katika ofisi yetu; iende ikafanye uchunguzi wa haraka, *by next week* tuweze kupata majibu halisia. Lengo kubwa tulinde fedha za walipa kodi wa Tanzania na hatimaye ziweze kusaidia wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuyajibu maswali yake kwa pamoja kwa muktadha wa namna hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Simbachawene majibu ya nyongeza.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri Jafo, lakini *concern* iliyooneshwa na Mheshimiwa Mbunge ni kubwa na kwa sababu hiyo basi kwa kuwa pia taarifa zetu zinakuwa tofauti na alizonazo, nimuombe baada ya kipindi cha maswali aje ofisini kwetu tuweze kupata taarifa zaidi, kwa sababu jambo hili ni la muda mrefu na bahati mbaya yule Mkurugenzi aliyekuwa pale sasa hayuko pale, lakini kesi ipo na inaendelea. Pengine kwa hatua hii sasa tunahitaji kwenda kwa haraka zaidi kulingana na *concern* aliyoonesha Mheshimiwa Mbunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni kweli kwamba kumekuwa na maamuzi mabaya kwenye Halmashauri yenye lengo la kutaka kuzitafuna fedha fulani kama zipo ambayo chanzo chake huwa ni kubadilisha matumizi. Waheshimiwa

Wabunge mimi napenda niwasihi sana, mabadiliko ya matumizi ya fedha za miradi zinazoletwa kwenye Halmashauri yanafanywa na Waheshimiwa Madiwani na vikao vile vinaridhia. Kupitia mwanya huo basi yanayotokea ni mambo ya ajabu. Kuna watu wamebadilisha hela ya mradi ambayo fedha inatolewa na *World Bank* wamekwenda kufanya yao, wamegawana posho, wamelipana vitu vyatya ajabu na wamepeana safari.

Mheshimiwa Spika, sasa kuanzia sasa uamuzi tuliofanya sisi kama Wizara ni kwamba mabadiliko ya matumizi ya fedha yoyote itabidi na Katibu Mkuu - TAMISEMI aridhie. Kwa sababu yanayofanywa huko ni mambo ya ajabu sana, kuna watu wanabadili fedha lakini kubadili huko ni kwa lengo la kwenda kutaka kuzitafuna. Kwa hiyo, sisi Serikali ya Awamu ya Tano hatutakubali jambo hilo liendelee kutokea. Niwasihi Waheshimiwa Wabunge mtusaidle kwa sababu na ninyi mnakuwepo kwenye vikao hivyo. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mary Nagu swali la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitashukuru sana kama TAMISEMI itakwenda kujua ukweli ni nini. Swali langu ni kwamba shule zile zilizotajwa za Katesh, Gendabi, Balangdalalu na Bassodesh sasa hivi kwa muda mrefu hazijapewa hela za chakula na ni shule za bweni. Taarifa hizo nimezififikasiwa kwa Mawaziri, nataka kujua, je, watoto waendelee kukaa bila chakula au kuna hatua ambazo zimechukuliwa? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hili Naibu Waziri wa TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ni kweli siku ya Mei Mosi tulikuwepo pale Katesh na Mama Mary Nagu na alililetu

tena jambo. Hata hivyo alilifikisha ofisini kwetu na ofisi ya Naibu Katibu Mkuu Elimu ilikuwa inashughulikia jambo hili. Kwa hiyo Mama Mary Nagu naomba vuta subira, tunadhani jambo hili linafikishwa mahali pazuri. Nadhani tutahakikisha kwamba watoto wale wanaweza kupata huduma kama ulivyopeleka katika maombi yale. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii 470 la Mheshimiwa Cosato David Chumi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Na. 470

Kutumia Mchezo wa Riadha Kutangaza Utalii

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Wanariadha wa baadhi ya nchi ambazo kijiografia mazingira yao yanafanana na baadhi ya maeneo katika nchi yetu wamekuwa wakishiriki katika mashindano ya riadha ya majiji makubwa duniani kama vile *New York Marathon, Tokyo Marathon* na kadhalika na hivyo kuzitangaza nchi zao ipasavyo.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa inafufua mchezo wa riadha ili kutumia kutangaza utalii wa nchi yetu?

NAIBU AZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya nchi zimekuwa zikifanya vizuri katika mashindano makubwa duniani na hivyo kuzitangaza nchi zao ipasavyo. Hata hivyo, nchi yetu imeanza kufanya vizuri katika mashindano ya riadha kama ilivyokuwa katika miaka

ya nyuma kupitia kwa wanariadha wake kama vile Francis Naal, Samson Ramadhani, Gidamis Shahanga, Juma Ikangaa, Suleiman Nyambui na Filbert Bayi. Mathalani, nchi yetu imeweza kupata mafanikio katika riadha hivi karibuni kupitia wanariadha wake kama ifuatavyo:-

(i) Alphonce Simbu aliyekuwa mshindi wa kwanza na kupata medali ya dhahabu kwenye mashindano ya *Standard Chartered Mumbai Marathon*, India tarehe 15 Januari, 2017;

(ii) Cecilia Ginoka Panga aliyeshinda Beijing *International Half Marathon* yaliyofanyika tarehe 16 Aprili, 2017; na

(iii) Emmanuel Giniki Gisamoda aliyeshinda *Shanghai International Half Marathon* yaliyofanyika tarehe 23 Aprili, 2017.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuleta maendeleo endelevu ya mchezo wa riadha na michezo yote kwa ujumla, pamoja na mambo mengine, Wizara inakamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 ili kuhakikisha inaendana na mahitaji ya sasa katika maendeleo ya michezo ikiwemo kuimarisha uendeshaji na usimamizi katika ngazi zote, ugharamiaji pamoja na uibuaji na uendelezaji wa vipaji katika ngazi mbalimbali.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendesha mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA ambayo pamoja na mambo mengine, yanalenga kuibua na kuendeleza vipaji vya vijana wetu katika mchezo wa riadha. Aidha, hivi sasa Wizara yangu inakamilisha taratibu za kuandaa miongozo ya Kiserikali ili kuwezesha wadau wote kuendesha kuendesha shughuli zao katika mazingira ya weledi na stadi bora za michezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia kwa kushirikiana na wadau inatekeleza programu mbalimbali za kuendeleza

mchezo wa riadha nchini ikiwemo *Kilimanjaro Marathon*, *Bagamoyo Marathon*, *Tulia Marathon*, *Heart Marathon* na kadhalika ambayo hushirikisha wanarisha kutoka ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Cosato Chumi; maswali ya nyongeza ni kwa wachezaji tu, sasa wengine mnasimama hata mazoezi hamfanyi. Mheshimiwa Cosato Chumi swali la nyongeza. (*Kicheko*)

MHE. COSATO DAVID CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Mwakyembe nillmuona ameenda kumtembelea yule nahodha wa *Serengeti Boys* ambaye aliumia wakati wa mashindano ya Gabon. Hilo ni jambo jema maana linawatia moyo sana vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wakati Alphonce Simbu anakwenda kushiriki mashindano kule *London Marathon*, kati ya magumu aliyokutana nayo ni suala zima la yeye kusaidiwa katika kupata *visa*. Simbu aliondoka hapa Alhamisi kuititia Afrika Kusini na kwenda kushiriki mashindano siku ya Jumapili, kitu ambacho kilimuathiri sana katika *performance* yake. Kama angeweza kuondoka mapema maana yake angeweza hata kuwa mshindi kuliko kushika nafasi ya tano. (*Makofi*)

Swali, je, Serikali iko tayari kuwasaidia wanariadha ambaao wame-*qualify* kwenda kushiriki mashindano makubwa ya Kimataifa katika kuhakikisha kwamba wanapata *visa* kwa wakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kama nilivyosema, mchezo wa riadha hasa katika kushiriki mashindano makubwa ya marathon kwa mfano, *Tokyo Marathon* inavutia

watazamaji wa barabaranı yaani wakati mbio zinakimbiwa kiasi cha watu milioni 1.7. *London Marathon* watu 800,000 wanakuwa wanashuhudia barabaranı, *Boston Marathon* watu milioni moja.

Swali, je, Serikali ipo tayari kugharamia maandalizi ya wanariadha wetu ambao wanakuwa wame-*qualify* kwenda kushiriki mashindano haya makubwa ambayo kwa namna moja au nyingine watasaidia kutangaza Taifa letu katika utalii? (*Makof*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Anastazia Wambura tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kupokea pongezi za Mheshimiwa Waziri wangu Dkt. Harrison Mwakyembe kutoka kwa Mheshimiwa Chumi, nitamfikishia salamu hizi. Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Chumi, kwa kujali kanuni na kujikita katika maswali ambayo yapo ndani ya swali la msingi, ambayo yanahusu riadha, namshukuru sana na ninampongeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Vile vile nimpongeze sana kwa sababu yeye ni mwanariadha wa vitendo, kila siku asubuhi huwa tunakutana naye katika uwanja wa Jamhuri akikimbia. Nina imani kabisa kwamba sasa hivi anaweza akawa anakidhi vigezo vya mashindano ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane naye kwamba kweli huyu Alphonse Simbu wakati anakwenda katika mashindano ya London alipata matatizo ya kupata

visa. Hata hivyo baadaye alifanikiwa kutokana na Serikali kuingilia kati zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwamba, mashindano haya huwa yanasmamiwa na vyombo mbalimbali. Kuna yale mashindano ambayo yanasmamiwa na *International Federations* lakini yapo mashindano ambayo yanasmamiwa na *Olympic Committees*. Kwa mfano, yapo mashindano ambayo yanasmamiwa na Shirikisho la Riadha la Taifa, lakini pia mashindano ambayo yanasmamiwa na *Tanzania Olympic Committee (TOC)*. Sasa haya ni yale ya Jumuiya ya Madola na yale ya *Olympic*. Ukiangalia mwanzoni Simbu hakupata matatizo wakati wanakwenda kwenye mashindano ya *Olympic*, ni kwa sababu hii *TOC* ilifanya maandalizi mapema.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mashindano yake ya pili ni kwamba alichelewa na kwa maana hiyo, napenda kutoa wito kwa wanariadha wote ambao wanapata sifa au vigezo vya kushiriki mashindano yoyote ya kimataifa au kupata mialiko yoyote ya kushiriki mashindano ya kimataifa, wale mawakala au mameneja wao au mashirikisho au pengine vyama, tunavishauri viwasiliane na Serikali mapema ili kusudi Serikali iweze kufanya mipango na kuwasiliana na maafisa wetu wa Ubalozi na kuondoa usumbu huu ambao ameusema; kwamba wakati mwingine unasababisha mtu kutokufanya vizuri. Kwa hiyo Serikali tukipata taarifa mapema, tunaweza tukasaidia kwa haraka sana ili kusudi mshindanaji na mchezaji ule aweze kupata *visa* mapema.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linauliza kama Serikali ipo tayari kugharamia maandalizi. Maandalizi kimsingi yanafanywa na vyama, vilabu na mashirikisho. Kwa kuzingatia kwamba michezo hii ni mali ya jamii na wanamichezo wenyewe wanatokana na jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nirudie tu kusema kwamba maandalizi yanapofanyika mapema, na hasa ile mipango ya vyama au mashirikisho, inapotufikia Serikalini mapema inakuwa ni rahisi kwetu kujua wale wamekwama wapi,

wanamikakati gani na hivyo tunaweza tukasaidia katika maandalizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tu niseme kuna wanariadha ambao wanatarajia, wanavigezo vya kwenda kufanya mashindano ya *Common Walk Games Australia* mwezi wa nne ambapo wako sita. Tumeshaanza kufanya mazungumzo na Serikali ya Ethiopia ili kusudi waweze kuweka kambi ya miezi nane kule Ethiopia na kupata utaalalm na kuweza kufanya vizuri katika mashindano hayo. Hata hivyo tuko katika utaratibu wa kutafuta vyanzo endelevu vya mapato ili kuweza kuwasaidia wanamichezo wote siku za baadaye. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Aaaaa! Sijaona mwana michezo wa *Bunge Sports Club* hata mmoja. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, swali la Mheshimiwa Shally Raymond.

Na. 471

Ongezeko la Bidhaa Bandia Nchini

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Kuna ongezeko la bidhaa bandia na zisizo na viwango zinazoingizwa nchini, miongoni mwa bidhaa hizo ni pembejeo za kilimo, madawa ya mifugo, dawa za binadamu, vyakula, vinjwaji, vifaa vya nyumbani na kadhalika.

(a) Je, ni hasara gani imepatikana kwa mwaka mmoja uliopita kutokana na bidhaa hizo kuingizwa nchini na kutumiwa na wananchi?

(b) Je, ni hatua gani zinachukuliwa kukomesha bidhaa hizo kuingia nchini hasa maeneo ya vijijini ambako uelewa wa watumiaji ni mdogo na maafisa wadhibiti ni wachache?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y.
WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Shally Josephine Raymond, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Tume ya Ushindani (*FCC*) na kwa kushirikiana na wamiliki wa nembo za biashara, inaendelea kudhibiti bidhaa bandia zisiingie nchini ili kuhakikisha ushindani wa haki katika biashara. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2016 Tume ya Ushindani ilikamata bidhaa bandia zenye thamani ya shilingi bilioni 18.67. Bidhaa hizo zilikamatwa kwenye kaguzi za bandarini, vitengo vya makontena (*ICDs*) na katika masoko.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) kwa kushirikiana na Taasisi nyingine waliteketeza bidhaa mbalimbali zenye thamani ya shilingi bilioni 2.4. Bidhaa hizo ni pamoja na nguo, nyama na *sausage*, vilainishi vya injini, *battery* za magari na za *solar* 1,430.

Mheshimiwa Spika, shirika pia liliifanya ukaguzi wa mabati na kutekeleza mabati 84,000 ambayo hayakukidhi viwango. Aidha, takriban lita 94,869 za vilainishi vya injini, na katoni 200 za bendera za Taifa zilirudishwa nchi zilikotoka. Vilevile aina 11 za pombe kali katoni 123,942 zilizofungashwa kwenye vifungashio vya plastiki vilizuiliwa kuingia sokoni na kurudishwa katika nchi zilikotoka.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Ushindani na *TBS* zinafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi nyingine katika kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kudhibiti bidhaa zinazopitia katika mipaka na nchi jirani, kufuatilia ubora wa bidhaa hafifu na bandia na kuziondoa katika soko. Ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa taasisi hizi, Serikali inongeza ajira za watumishi, kufungua vituo vya ukaguzi wa bidhaa katika mipaka yote na kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya

habari kama vile luninga, redio na magazeti na kushirikiana na vyombo vyatuzi na usalma kuzuia magendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote tushirikiane kupambana na bidhaa bandia na zisizokidhi viwango. Adui namba moja wa viwanda ni bidhaa bandia na zile zisizokidhi viwango.

SPIKA: Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante; nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya ufanuzi. Kwa kuwa tumeshuhudia kwenye luninga wakiteketeza vifaa hivi na wanaoingiza kupata hasara, Je, ni hatua gani zaidi zinazochukuliwa kwa wale wanaoingiza ili kukomesha hali hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vifaa bandia havitoki tu nje ya nchi, vingine vinatengenezwa humu humu nchini. Mimi naomba kujuua ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali ili kukomesha kabisa vifaa hivyo, vikiwemo viatilishi, pembejeo za kilimo, vipodozi vyta kina mama, na hata vingine ambavyo si rahisi kutamka hapa hadharani? Naomba kujuua. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya naswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer Isack Kamwelwe*.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza nakiri na amekubali jibu kwamba kweli vile vifaa vinateketezwa na yeye mwenyewe ameona; lakini ni hatua gani zinachukuliwa sasa kwa wale ambao wameshikwa na hizo bidhaa bandia.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, tunazo sheria nchini, yule anayeshi kwa na vifaa bandia ni kwamba anapata stahili kulingana na sheria. Wakati mwingine wanatozwa faini na pengine inaweza hata zaidi ya hiyo akapewa adhabu stahiki.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili amesema kwamba hivi vifaa bandia sio kwamba vinatoka nje ya nchi tu, kuna vingine vinatengenezwa humu ndani. Kwa mfano, kama vipodozi wapo watu wanachanganya vipodozi na wamewaathiri sana wale ambao wanatumia.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kufunga viwanda vile ambavyo havijasajiliwa na mara nyingi hivi vitu ambavyo vinafanywa ambavyo havipo katika viwango vinafanywa na viwanda bubu. Kwa hiyo, Serikali inafanya ukaguzi, kama tulivyojibu katika swali la msingi ili kuhakikisha kwamba hawa wote wanaofanya hivyo wanakamatwa na wanapewa adhabu stahiki kwa mujibu wa sheria na viwanda vinavyojihuisha na hivyo tayari vinafungwa ili kuhakikisha kwamba suala hilo haliendelei. Vilevile pia nimeongea na Mheshimiwa Waziri akasema kwamba wanatarajia kuleta sheria itakayotoa adhabu kali zaidi hasa kwa hawa watu ambao wanatengeneza vitu bandia.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Magdelina sakaya, Kamishna, swali la nyongeza.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa vifaa vyaa bandia kwenye maduka sasa hivi siyo siri tena, hata ukienda wanakwambia kuna hiki hapa ambacho ni dhaifu, kuna hiki hapa na bei pia ni tofauti. Kwa hiyo si kwa njia ya vichochoroni hata madukani viro na vinauzwa halali kabisa.

Je, Serikali haioni, kuruhusu kuwepo kwa bei aina mbili/tatu kwenye kifaa kimoja dukani ni kuruhusu kuwepo kwa vifaa bandia kihalali kitu ambacho tunapiga marufuku katika nchi yetu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer Isack Kamwelwe.*

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI): Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri ni kweli, unakwenda dukani unakutana na hiyo hoja. Na hoja yenyewe inakuwa kwenye kukata mapato kwenye *TRA*, na ndio maana juzi juzi hapa, kama umeongea na wafanyabiashara *TRA* imeendelea kuweka sheria ngumu ikiwepo pamoja na kila duka hata kama ni dogo lazima liwe na ile mashine ya *EFD* kwa ajili ya kupata zile *recept* ili waweze kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara ya Fedha inaendelea kuweka sheria kali na ukaguzi mkubwa sana katika bidhaa. Suala moja ambalo ni zuri kwa sisi Waheshimiwa Wabunge ndugu zangu tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu. Sasa kama wewe unapewa hiyo kauli, kwamba ukitaka bidhaa hii itakuwa na shilingi kadhaa lakini hii itakuwa na bei chini zaidi, wewe mwenyewe lazima ujiulize kwamba kwa nini hii ni chini?

Mheshimiwa Spika, kama ningelikuwa ni mimi ningeweza nikasema basi naomba uniuzie hiyo hiyo ya bei ambayo ni kubwa lakini unipe *receipt*. Kwa sababu hiyo moja kwa moja ameshakwambia hii haina ubora, sasa wewe kwa nini uende ukununue.

Mheshimiwa Spika, lakini nakiri pia kwamba, si wananchi wote wa Tanzania hasa vijijini wenye elimu ambayo naweza nikawa nayo mimi au unaweza ukawa nayo Mheshimiwa Sakaya. Sasa ni suala letu sisi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani na Serikali kwa pamoja tuendelee kuwaelimisha wananchi ili waweze kukwepa haya na ndio maana Serikali sasa inaweka viwanda nya ndani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba hata viwanda nya ndani nao wanaweza wakafanya vitu nya namna hiyo. Ndugu zangu tunayo kazi kwa hiyo tuendelee

kuelimisha jamii na kutunga sheria zilizo kali na tuzisimamie ili haya yaweze kuondoka.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Wizara, swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbaruku, Mbunge wa Jiji la Tanga kwa niaba yake.

Na. 472

**Kufanya Usajili wa Abiria na Kupima Mizigo Vyombo
Vyote veya Majini**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y. MHE. MUSSA B.
MBAROUK)** aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa majini, mizigo na watu havifanyi usajili na vipimo.

Je, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kupima mizigo na usajili wa abiria katika vyombo vyote kama wanavyofanya Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCCAA*) ili kuepusha ajali za mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa aina mbili unaotumika kupima mizigo na usajili wa abiria katika vyombo vinaavyotumika majini. Kwanza usajili na uorodhesaji wa mizigo wakati wa ukataji wa tiketi za abiria na upakiaji wa mizigo kama inavyoainishwa katika *passenger or Cargo Manifests and Crew List*. Pili, uhakiki wa upakiaji kabla ya chombo kuruhusiwa kuanza safari, kwa kuhesabu abiria wakati wa kuingia kwenye chombo na kuhakiki kuwa alama ya *Loading Mark* haivukwi. Aidha, matumizi ya *Port*

Clearance Forms huwezesha kudhibiti kiwango cha upakiaji abiria na mizigo kwenye chombo na kuacha taarifa za safari.

Mheshimiwa Spika, Serikali hufanya udhibiti huo, kupitia mamlaka ya udhibiti usafiri wa nchi kavu na majini (*SUMATRA*) na mamlaka ya usimamizi wa bandari *TPA* ambazo husimamia utaratibu wa upakiaji bandarini na kudhibiti usalama wa vyombo vyta usafiri majini. Taratibu hizi hufanywa au hatakiwa kufanywa kwenye bandari na mialo yote iliyosajiliwa.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Temeke, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Spika nakushukuru kunipa nafasi na mimi kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kabisa kwamba kuna mialo ambayo haijasajiliwa na inasafirisha abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Nataka kujua Serikali kupitia *SUMATRA* na *TPA* wanatumia utaratibu gani kuhakikisha kwamba vipimo vyta kuhakikisha kwamba mizigo na abiria wanaoingia kwenye vyombo vyta usafiri vinakwenda sambamba na uwezo wa chombo?

Mheshimiwa Spika, swali la pilli, bado kuna vyombo vingi vibovu na visivyokuwa na *life jacket* vinafanya safari za kubeba abiria kutoka Pwani ya Tanga kwenda Pemba; kutoka Pwani ya Dar es Salaam kwenda Unguja na kutoka Pwani ya Mkoa wa Pwani kwenda Mafia na sehemu zingine za jirani kama visiwa vyta Comoro. Vyombo hivi vinafanya safari usiku vingine vinapotea na hata kumbukumbu hatuna. Serikali ina mpango gani wa kudhibiti safari za usiku za vyombo vibovu vinavyosafirisha abiria ili visiweze kufanya hivyo kunusuru maisha ya Watanzania?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi kwamba vyombo vyote vyta majini kuanzia

wakati vinatengenezwa kuna *loading mark* huwa inawekwa yaani chombo kikielea majini hakitakiwi ile *loading mark* izame chini, hicho ndicho kitu cha kwanza ambacho vijana wa *SUMATRA* wanakitungia katika kuhakikisha kwamba chombo hiki kinachokwenda kuelea majini na kusafirisha abiria na mizigo hakijazidisha abiria wala mizigo, kwa kukagua ile *loading mark*.

Mheshimiwa Spika, pili kuhusu suala la ni namna gani tunaweza kudhibiti, na vile vile vyombo hivi vinavyosafirisha abiria kati ya Tanga, Dar es Salaam na Zanzibar tunavidhibiti vipi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vijana wetu wa *SUMATRA* wapo katika mialo, mialo ile iliyosajiliwa. Labda tu nichukue fursa hii kukiri na mara nyingi nakiri kwamba kuna mialo ambayo haijasajiliwa, na mingine hatujui.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo ndiyo maana tumeweka usimamizi kwa kutumia viongozi wetu kamati za ulinzi na usalama za Mikoa yote ya Pwani na Zanzibar wanakutana kila baada ya miezi, na wakati mwagine miezi sita wanakutana na mikoa mbalimbali katika hii mikoa ya ukanda wa Pwani pamoja na Zanzibar ili kujadili na kuhakikisha kwamba wanaitambua ile mialo yote ambayo haitambuliki. Mialo hiyo ndiyo inayotumika mara nyingi kusafirisha mizigo usiku bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, niwaombe tu nanyi Waheshimiwa Wabunge tuhamasishe watu wetu wasitumie hii mialo ambayo haijasajiliwa, kwa sababu kwanza ni hatali lakini pili inapoteza mapato yetu kwa sababu hii mialo tunaitumia vilevile kukusanya kodi zinazotusaidia kuleta huduma mbalimbali za jamii na kufanya shughuli mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana tusaidiane ili kuhakikisha mialo hii ambayo inaoparate *illegally* tuidhibiti kwa pamoja tukishirkirikiana na nyinyi Waheshimiwa Wabunge, muwaelimishe watu wenu. Kwa sababu hatimaye hawa watu wanatoka katika maeneo yetu. (*Makofii*)

SPIKA: Kwa kuwa swali linahusu vyombo vya majini nadhani nisipompa Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Mbaraka Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa abiria na mizigo katika bandari ya Kilindoni kwa zaidi ya miezi mitatu sasa iko mashakani kufuatia kukatika kwa ngazi katika gati la Kilindoni. Abiria wanalahazimika kupanda kwa kutumia mitumbwi na viboti vidogo vidogo kwenda kupanda boti kubwa hali ambayo ni hatari sana kwa usalama wao.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatuhakikisha Wananchi Mafia kwamba atawaelekeza watu wa Mamlaka ya Bandari waje watengeneze warekebishe gati lile illi lianzesha kutumika? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, ninafahamu umuhimu wa usafiri wa majini kwa ndugu zetu wa Mafia, ni njia kuu kwa wale ambao hawana uwezo wa kutumia ndege na kwa sababu hiyo nawaagiza *TPA* wafanye haraka sana kwenda Mafia pale Kilindoni ili lile daraja ambalo limekatika liweze kurekebishika na hatimaye ile gati iweze kuanza kutumika kwa kutoa usafiri kwa ndugu zetu wa Mafia.

SPIKA: Mheshimiwa Saumu nilikuona, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. SAUMU H. SAKALA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la ukaguzi katika vyombo vya majini kwa kweli bado halifanywi kwa asilimia 100, hasa

nikzungumzia katika bandari ambazo ziko katika Wilaya zetu *SUMATRA* hawana ofisi katika kila Wilya ambazo ziko Pwani.

Nikzungumzia Pangani hakuna ofisi ya *SUMATRA* na badala yake *SUMATRA* wamekabidhi madaraka yale kwa watua wa *TRA* ili waweze kuwakagulia vyombo ambavyo vinasafiri. Pamoja na hayo *TRA* hawana wafanyakazi wa kutosha jambo ambalo wakati mwingine wakati chombo kinasafiri, iwe ni usiku au ni mchana, unakuta *TRA* hayuko pale kwa ajili ya kukagua kile chombo. Kwa hiyo chombo unakuta kinajaza kuliko uwezo wake na ndivyo hivyo vyombo ambavyo vinapoteza muelekeo Baharini vinapata ajali watu wanakufa na hatujui idadi ya watu waliokufa wala mizigo inayopotea.

Mheshimiwa Spika, nizungumzia Bandari ya Pangani mizigo mingi sana inapotea kutokana na hiyo hali na watu wengi wanakufa kutokana na hiyo hali na hawatangazwi. Sio hilo tu kuna zile bandari ambazo ni bubu, bado hazina kabisa usimamizi na watu wamekuwa wakipoteza maisha pamoja na mizigo. Sasa ni lini Serikali itachukulia kwa umuhimu wake suala hili la usafiri wa majini ambao umekuwa ukipoteza maisha ya watu bila kugundulika ili ajali hizi ziweze kupungua? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Engineer Ngonyani.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la swali la msingi kwamba *SUMATRA* wamepewa mamlaka ya kusimamia bandari zetu zote na bandari zote ambazo zimesajiliwa. Nakiri kwamba kuna bandari zingine ni bandari bubu na huwa zinazuka kila wakati, ni bandari ambazo zinatumika na wahalifu, kwa sababu kila ukiwadhibiti hapa wanaenda kutafuta sehemu nyingine. Ni wahalifu kwa sababu wanakiuka sheria za shughuli za bandari zinazosimamiwa na *SUMATRA* na kila tukiaribu kuwaelimisha, kwamba jamani acheni kutumia bandari

bubu mtumie bandari ambazo zimesajiliwa rasmi, bado tunakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine kama tutataka *SUMATRA* iwe katika kila aina ya bandari inayozuka kila wakati uwezo huo tutakuwa hatuna. Niwaombe sana Waheshimwa Wabunge tusaidiane, tuhakikishe mizigo yetu ipite katika zile bandari ambazo ni rasmi, tuache kupitisha katika bandari bubu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukabidhi kazi za *SUMATRA* kwa upande wa *TRA* au hata taasisi nyingine, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo *TRA* inaona kwamba zile kazi zimewazidi huwa wanarudi kwetu, kwa maana na *SUMATRA* na kuwaambia kwamba hapa tunahitajika tuwe na *permanent station* ya watu wa *SUMATRA* na hatimaye huwa tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yale ambayo *traffic* si kubwa sana tunawatumia wenzetu wa *TRA* na sehemu zingine *TPA* wanatumika kutegemeana na jinsi ya kutumia *resources* za Serikali tulizonazo. Sidhani kama tutaweza kwa *SUMATRA* peke yake kusimamia kila bandari tulizonazo, kuweka idadi ya staff inayotakiwa. Tunatumia taasisi zingine kufanya kazi hizo kwa kushirikiana na tasisi hizo zinawasiliana muda wote kuhakikisha kwamba pale ambapo panapolamika kuweka *permanent station* ya *SUMATRA* hatimaye tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nirudie tena. niwaombe sana ndugu zangu, na hasa ninyi wenzetu mnaotoka katika maeneo ya ukanda wa Pwani mtusaidie ili watu wetu wafuate sheria na Sheria za *SUMATRA* na Sheria za *TPA* ni sheria mama kama zilivyo Sheria zingine, si kwamba zile Sheria ziko kiwango cha chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kila mmoja ana uwezo wa kuzivunja kwa kadri anavyoona inafaa. Niwaombeni sana tusaidiane ili tuhakikishe kwamba maisha ya wananchi

wetu na mizigo yao haiathiriwi katika safari za baharini na kwenye maziwa.

SPIKA: Tunaendelea na swali la Mbunge wa Manonga, Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali kwa Wizara hii hii ya Uchukuzi.

Na. 473

Mnara wa Mawasiliano- Jimboni Manonga

MHE. SEIF K. GULAMALI aliuliza:-

Tanzania tuna ushindani mkubwa wa Kampuni za Simu na katika Jimbo la Manonga maeneo kama ya Kata ya Mwashiku, Ngulu, Kitangari, Sungwizi, Mwamala, Uswaya, Tambarale na Igoweke hayana minara ya mawasiliano.

Je, ni lini Serikali itazielekeza Kampuni za Simu kusimamia minara yao kwenye maeneo ambayo hayana mtandao wa mawasiliano?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa maeneo ya Kata za, Mwashiku, Ngulu, Ntobo, Kitangiri, Sungwizi, Mwamala, Uswaya, Tambarale na Igoweke hayana minara ya mawasiliano. Serikali kuititia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uliyaanisha maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Igunga, hususan Jimboni Manonga na kuyaingiza kaitka utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Matinje na Mwashiku kutoka kata ya Mwashiku, vijiji vya Imaiilo na Mwasung'ho kutoka katika kata ya Ngulu, kijiji cha Mwamloli kutoka katika kata ya Ntobo na vijiji vya Igoweke na Uswaya kutoka kata

ya Igowecko vitafikishiwa huduma ya mawasiliano kupitia utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa Viettel unaotarajiwu kukamilika Novemba, 2017. Aidha, vijiji ya Kitangiri kutoka Kata ya Ndembezi na vijiji vya Sungwizi na Mwamala kutoka Kata ya Sungwizi vimeingizwa katika orodha ya miradi inayosubiri upatikanaji wa fedha ili kutekelezwe, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Manonga swali la nyongeza.

MHE. SEIF K. GULAMALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; nina maswali (a) na (b).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kuwa kati ya kata 19 zilizoko ndani ya Jimbo la Manonga kata tisa hazina mawasiliano, kwa maana ya vijiji vyote vilivyoko ndani ya zile kata tisa, je, Serikali haioni kuwa katika maeneo hayo wananchi hawatendewi haki kwa sababu wanakosa mawasiliano? Na je, Serikali kutokana na majibu yake inatuhakikishiaje kuwa mpaka Novemba itakuwa tayari maeneo hayo yamepata minara ya simu katika maeneo yaliyotajwa?

Mheshimiwa Spika, swali b je Waziri atakuwa tayari tuongozane naye ili awezekwenda kujionea hizo kata ambazo hazina mawasiliano ya simu? Kama yuko tayari ni lini ili aweze kuona adha ambazo wananchi wanazipata? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kwenye jibu la msingi Serikali inakiri kuwa kati ya kata 19, kata 10 zinamawasiliano na kata tisa hazina mawasiliano. Kwetu sisi hayo ni mafanikio makubwa na tutahakikisha kata tisa zilizobaki ambazo ni chini ya asilimia 50 tunazifikisha mawasiliano katika kipindi hiki cha miaka mitano itakapofika

mwaka 2020 hilo litakamilika na tutalikamilisha kwa kutumia mkataba tulionao na kampuni ya Viettel kwa kuwa tuna mkataba nao, lakini vilevile Mfuko wetu wa Mawasiliano kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge umefika ofisini tumekutana na wataalam, bahati nzuri hivi vyote tuliviorodhesha na sasa unafahamu, labda ni vizuri tu na wananchi wako wakafahamu kwamba kata hizo zote tisa tumeshazichukua na tutazifanyia kazi katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kufika katika eneo lake na kuzipitia hizo kata.

Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka ndani ya Bunge lako Tukufu alipouliza swalı lake la nyongeza nilimjibu kwamba mimi siamini kijiji kama Machinja hakina mawasiliano kwa sababu watu ni wengi sana. na nitumie nafasi hii kuyafahamisha makampuni ya simu tunamaeneo mengi yenye watu wengi sana, mahala ambapo pana biashara kubwa. Maeneo hayo hatuhitaji fedha ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote yaende katika maeneo hayo. Kwa sababu maeneo hayo ni yakibiashara, yana watu wengi na mkipeleka mawasiliano mtapata fedha za kutosha. *Its economically viable.*

Kwa hiyo karibuni sana Waheshmiwa Wabunge tupeane taarifa maeneo ambayo yana watu wengi sana center kubwa sana makampuni yenye yaende tusitumie hela zetu za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Hela hizi za mfuko wa mawasiliano kwa wote tuzitumie katika maeneo ambayo hayavutii kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nitakuja katika lengo hilo hilo la kuhamasisha makampuni kwanza yaje, lakini pili tuone *UCSAF* itafanya je kazi kama ambavyo tulikuahidi ulipofika ofisini na tukakutana na wataalam. Hongera sana Mheshimiwa kwa kufuatilia suala hili kwa umakini sana.

SPIKA: Kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge mkiangalia muda wetu twende Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi swali linauliza na Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki. Mheshimiwa Mtuka.

Na. 474

Umuhimu wa Kulitambua Eneo Lenye Alama Pekee Katikati ya Tanzania

MHE. DANIEL E. MTUKA aliuliza:-

Taarifa ya Idara ya Upimaji wa Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inalitaja eneo la Chisinjisa liliopo Wilaya ya Manyoni kuwa ndipo alama pekee ya katikati (*center point*) ya Tanzania inapatikana.

(a) Je, ni lini Serikali italitambua rasmi eneo hili na kulitangaza katika Gazeti la Serikali?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuendeleza na kulitangaza eneo hili ili kuvutia utalii wa ndani na nje kama chanzo cha mapato?

NAIBU WAZIRI WA ARIDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swali namba 474 kutoka kwa Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna taarifa rasmi za kitaalam zilizobainisha kwamba Kijiji cha Chisinjisa ndipo alama pekee ya katikati (*center point*) ya Tanzania pamoja na wenyeji wa eneo hilo kudai kuwepo kwa alama hiyo eneo la Sukamahela.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Upimaji na Ramani inakusudia kufanya utafiti wa kina kwa kutumia elimu ya jiometriki (*geometrics*) ili kubaini eneo rasi ambalo alama ya katikati (*center point*) ya Tanzania inapatikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya utafiti huo kukamilika eneo la katikati ya Tanzania litatangazwa katika Gazeti la Serikali. Aidha, mamlaka zinazohusika na masuala ya utalii zitaliendeleza eneo husika ilikuvutia utalii wa ndani na nje kama zinavyofanya nchi nyingine duniani na kuongeza mapato ya Serikali.

SPIKA: Mheshimiwa Daniel Mtuka, umeridhika?

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Huu ni ubunifu mkubwa na wa kupongezwa kwa wananchi wa Manyoni Mashariki kwamba tuwe na eneo sasa litambuliwe la katikati ya nchi, na kwa sababu taarifa za awali zinaonyesha kwamba eneo hili liko kwenye Manyoni Mashariki. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imeona umuhimu wa kulitambua, kulipima na kulitangaza eneo la katikati ya nchi kwa lengo la kukuza utalii; na kwa kuwa wananchi wa Manyoni wako tayari kushirikiana na Serikali katika kuliendeleza eneo hilo pamoja na kujenga mnara mrefu ambao utawekwa taa au bendera ya Taifa.

Je, Waziri anaweza kutoa maelekezo sasa hivi hapa ndani amuagize Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani aanze kazi hiyo mara moja ya kulitambua eneo hili? (*Makofii*)

(ii) Kwa kuwa lengo kubwa hapa ni kukuza utalii na kuongeza vivutio vya watalii, tunayo hazina ya mali kale, kubwa eneo la Kilimatinde pale Manyoni.

Je, Waziri na Maliasili na Utalii atakuwa tayari kufuatana na Mbunge kwenda kuona eneo hilo ambalo ni

hazina kubwa ya kumbukumbu za biashara ya utumwa pamoja na ngome za wakoloni? (*Makofi*)

SPIKA: Kwa Waheshimiwa Wabunge msiofahamu jina la Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni Mashariki Mtuka kwa Kigogo maana yake ni gari. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Mtuka.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza amesema je, niko tayari pengine kutoa tamko hapa, ili Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani aende aanze kufanya kazi hiyo; nadhani katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Wizara sasa tayari inaweka mikakati ya kuweza kufanya ufatiliaji wa karibu, kwa sababu tumeona kuwa na eneo ambalo linatambulika kama ndilo *center* (katikati) ya nchi si tu kwamba tutatambua eneo hilo na kuliacha kama liliyo, lakini bado ni sehemu ambayo inaweza ikatumika pia kama utalii. Ndiyo maana nimesema uendelezaji wa eneo hilo, unaweza ukafanyika katika mustakabali wa kutaka patambulike.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu wananchi wa Manyoni Mashariki wanasesma wako tayari kushirikiana mara zoezi hilo litakapoanza tutawashirikisha kwa pamoja ili tuweze kuona suala lile linafanyika katika umakini zaidi ili kuweza kupafanya pawe kivutio cha kweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili la kuweza kutambua vivutio vilivyoko katika maeneo ya Kilimatinde, nadhani hili ni la Wizara ya Utalii, lakini kwa sababu wote tunajenga taifa moja, tutashirikiana na wenzetu kuweze kuona maeneo hayo yanatambulika na yanaingia katika historia, lakini pia kuweka kama vivutio vya utalii ili paweze kufikika pia na patakuza soko la utalii kwa nchi yetu.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, nilikuona majibu ya nyongeza.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni.

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Manyoni tunamshukuru sana kwa kutupa taarifa ya malikale hizo ambazo ziko katika eneo hilo na ninataka nimhakikishie kwamba tuko tayari kutembelea eneo hilo na kufanya kazi vivutio hivyo, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mtuka ujumbe wako umefika. Swali linalofuata 475 litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

Na. 475

Mpango wa Kuendeleza maeneo ambayo ni *Squatter*

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA aliuliza:-

Je, nini sera ya Serikali katika kubadilisha mandhari ya maeneo ambayo ni *squatter* au ya wazi kwa kuwekeza katika majengo ili kuwa na makazi ya kisasa kwa ajili ya wananchi kwa kutumia ardhi iliyopo katika eneo husika?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali namba 475 la Dkt. Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kifungu namba 4.1.4.2 cha Sera ya Taifa ya Makazi ya mwaka 2000 kinaelekeza kuwa maeneo yaliyojengwa bila kupangwa na kuwekewa huduma za msingi yaboreshwe na wananchi wenyewe kwa kushirikiana na asasi za kijamii. Kwa maeneo yaliyojengwa bila kupangwa na kupimwa lakini yapo katikati ya miji (*prime areas*) hususan katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara imeandaa rasimu ya

mkakati wa uboreshaji wa maeneo hayo kwa kutumia dhana ya kukusanya ardhi (*land pooling*). Utekelezaji wa dhana hii utawawezesha wananchi wa maeneo husika kupata makazi bora na pia kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji mpya.

Mheshimiwa Spika, dhana ya kukusanya ardhi inalenga kuboresha maeneo hayo kwa kujenga majengo makubwa ya ghorofa ili kuweza kuwapatia makazi mbadala wakazi wa maeneo husika katika eneo hilo hilo, na pia kupata eneo la uwekezaji utakaojumuisha ujenzi wa majengo ya kibiashara kama vile maduka makubwa (*super markets and shopping malls*), makazi ya maghorofa ambayo mengi yanakuwa na *apartments*, hoteli, huduma za kijamii, maeneo ya wazi, maeneo ya burudani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, rasimu hiyo kwa awamu ya kwanza inapendekeza kufanya ukusanyaji wa ardhi katika maeneo ya Manzese, Vingunguti, Buguruni, Msasani, Keko, Namanga, Mikocheni na Kawe.

SPIKA: Mheshimiwa Mary swali la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jiji la Mbeya halina *master plan, general plan scheme* na limekuwa katika *data collection* ya *almost* bilioni1.5. Swali langu ni kwamba je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa ku-*push* hili jambo lifike mwisho?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri walishatembelea katika Jiji la Mbeya na nilikuwa bega kwa bega, mguu kwa mguu na Mheshimiwa Naibu Waziri yeye mwenyewe amejionea ni jinsi gani Jiji la Mbeya limekuwa ni la *squatter* kwa muda mrefu sana, hususan katika maeneo ya Isanga, Illemi, Nzovwe, lyunga, Kalobe, Nonde, Mwakibete, Sinde, Soweto; yote haya

na mengineyo mengi ni *Squatterkwa* muda mrefu sana. Swali langu kwa Serikali, haioni kuwa sasa ni wakati muafaka tena wa kusaidia *up grading* katika maeneo hayo? Nakushukuru.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Angelina Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanjelwa kwa sababu mara nyingi katika Bunge hili kama tutakumbuka kila akileta swali la Makazi mara nyingi anapenda kutolea mfano wa Mbeya ambao unakuwa pengine haujawa na *master plan* mpaka dakika hii, lakini ni mji ambao unakuwa kwa kasi kubwa. Sasa hivi Wizara yangu inayo miji karibu 28 ambayo tayari michakato yake ya *master plan* inaendelea.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Mbeya bado halijawa, mimi niwaombe sana watu wa Mbeya tuanze maandalizi ya kuwa na *master plan* kwa sababu mchakato mzima lazima uanzie kwenye eneo husika. Ni wazi kama wataanzisha kama ambavyo miji mingine imeanza kama Arusha, Dar es Salaam na Mwanza ambayo imeishaanza, sasa mimi niseme tu kwamba Jiji la Mbeya nalo sasa linatakiwa lianze mchakato huo kwa sababu ni suala ambalo litafanya libadilishe kabisa mandhari ya mji wenywewe.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, ni kweli nikiri kwamba nilikwenda Mbeya na tuliongozana naye, na maeneo anayoyataja ni kweli hayavutii kwa kasi ya namna ambavyo ilivyo. Mimi nimpongeze kwa sababu pia, amekuwa na kiu ya kutaka kuona mabadiliko yanakuwepo.

Mheshimiwa Mwanjelwa naomba nikuhakikishie kwamba kwenye maeneo ya lyunga, Kalobe, Uyoe, Nondé, Mwakibete, Sinde, Isanga, Soweto na kadhalika, kweli nilijiona maeneo hayako katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niseme pale ambapo mtaanza *master plan*, basi tutawekeza pia katika maeneo

hayo kuhakikisha kwamba yanabadilika ikiwa ni pamoja na kubadili mandhari kama ambavyo ulivyoomba kuweza kufanya ile *pulling* ya *land* kuweza kuleta pamoja na kuweza kujenga majengo ambayo pengine yatapendeza zaidi au kuweka mandhari ambazo zitafanya ule mji kweli uonekane kweli ni Jiji.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaedelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na swali ni la Mheshimiwa Mbunge wa Tunduma, mpakani Mheshimiwa Mwakajoka.

Na. 476

Ada inayotozwa na Zimamoto (*Fire*) Tunduru

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na ada ya Zimamoto ambayo wanatozwa wafanyabiashara katika Halmashauri ya Mji wa Tunduru huku kukiwa hakuna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji eneo hilo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ada zinazotozwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kwa mujibu wa Sheria Na. 14 ya 2007 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Kanuni za Ukaguzi za mwaka 2008 na Marekebisho yake ya mwaka 2012 na 2014. Sheria na Kanuni hizi zinamtaka mmiliki wa chombo cha usafiri pamoja na usafirishaji, mmiliki wa jengo refu au fupi, chombo cha usafiri na usafirishaji, mfanyabiashara au ofisi kulipia tozo ya ukaguzi. Tozo hizo zimepangwa kutohana na ukubwa wa jengo na hatari ya moto kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Mombasa Mkoani Songwe, Halmashauri ya Tunduma ina kituo cha Jeshi la

Zimamoto na Uokoaji ambacho kipo katika Mtaa wa Kilimanjaro na kina askari kumi na gari moja la kuzimia moto. Kwa sasa gari hilo lipo Jijini Mbeya kwa ajili ya matengenezo. Wizara kuititia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inafanya jitihada za haraka ili gari hilo litengamae na kurejea kituoni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, askari wa Jeshi la Zimamoto na uokoaji wanaendelea na majukumu yao mengine ya kutoa elimu ya kinga na tahadhari za moto na ukaguzi wa majengo ili kuzuia ajali za moto na majanga mengine. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Tunduma swalii la nyongeza.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuiliza swalii la nyongeza. Kabla sijaauliza swalii la nyongeza ningependa nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Zambia kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya ya kuhakikisha kwamba wanatuazima gari yao ya Zimamoto kwa ajili ya kuzima moto kwenye mji wa Tunduma, ninasema *mwasalifya sana mwe wantu wa Kuzambia*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu la kwanza; najua kabisa kwamba Tunduma iko mpakani mwa Zambia na Tanzania na shehena kubwa sana ya mizigo inayoshuka kwenye bandari ya Dar es Salaam inapita Tunduma na Tunduma hatuna gari ya Zimamoto. Je, Serikali haioni kwamba inahatarisha maisha ya wana Tunduma lakini pia na mizigo inayopita kwenye mpaka wa Tunduma?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, wananchi wa Tunduma wanaendelea kutoa ada za zimamoto wakati huduma ya zimamoto kwenye Mji wa Tunduma haipo, hatuoni kama huu ni uzulumaji wa wazi kabisa wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa wananchi wa Tunduma kuendelea kutozwa fedha hizi bila kupata huduma ambayo ni muhimu katika maisha yao? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchembba.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika, kwanza alivyotoa shukurani hizi nikapata mashaka sana, maana mipakani kule kuna mwingiliano sana wa uraia na nilipoona sifa nyingi sana zinaenda Zambia nikataka kujua sana babu zake wake wako wapi. (*Makofi/Vicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri usipate taabu, hawa jamaa zetu chifu wao yuko huko huko. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika, lakini yote kwa yote ni kheri. Niseme tu kwamba yale aliyojasema Mheshimiwa Mwakajoka kwa utaratibu wetu, tungekuwa hatuna gari kabisa katika eneo husika ingekuwa ni hatari sana, lakini vitu hivi vya moto huwa vinaharibika, na kama nilivyojasma kimeenda matengenezo na baada ya hapo kitarudi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuwatoza hii ni kwa mujibu wa sheria na sheria za kodi za nchi yetu, si kila kodi inakwenda *specific* huduma kwa mtu aliyechangia kodi hiyo, na tukifanya hivyo tutakuwa tumekosea kwa sababu kuna maeneo mengine makusanyo ni kidogo.

Kwa hiyo, mimi nitoe rai kwa wananchi wetu waendelee kutoa kodi hizo na hivi tunavyoongea kwenye bajeti iliyopita tumepitisha bajeti ya magari mengine, tunategemea kupata magari mengine kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na huduma hiyo itasambaa katika maeneo mengi zaidi kama ambavyo tumepanga katika malengo yetu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Swali letu la mwisho kwa siku ya leo kwa sababu ya muda litaulizwa na Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu. Mheshimiwa Mwantakaje.

Na. 477

Hitaji la Gari la Polisi – Magharibi ‘A’

MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia gari lingine Kituo cha Polisi Magharibi ‘A’ ili kupunguza matumizi ya magari binafsi kwa Jeshi la Polisi?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kupunguza uhalifu unaojitekeza mara kwa mara?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Bububu lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la upungufu wa vitendea kazi katika Jeshi la Polisi hususan magari ya doria kote nchini ikiwemo Bububu. Kwa kuzingatia umuhimu wa doria katika kudhibiti masuala ya usalama wa raia, Serikali inaendelea kuongeza idadi ya magari na vitendea kazi vinginevyo kadiri hali ya uchumi inavyoruhusu. Mpango ya Jeshi la Polisi ni kupeleka gari moja katika Wilaya ya Magharibi ‘A’ mara baada ya kupokea magari mapya katika siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la ulinzi wa raia pamoja na mali zao ili kuhakikisha wananchi na mali zao wanakuwa katika hali ya usalama. Katika kutekeleza jukumu hilo ipo mikakati mbalimbali ambayo imetekelezwa ikiwa ni pamoja na kufanya doria na operesheni za mara kwa mara, kutoa elimu kwa jamii ili kuwajengea uwezo wa kutambua matendo yanayoashiria uhalifu na kutoa taarifa polisi kwa lengo la kuchukua hatua kabla uharibifu kufanyika. (Makof)

SPIKA: Mheshimiwa Mwantakaje swalii la mwisho la nyongeza kwa siku ya leo.

MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fungu la mafuta katika magari hayo linakuwa ni kidogo, je, ni lini Serikali itaongeza mafuta hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili katika Mkoa wangu wa Magharibi 'A' mafuta wanapokea kwa siku lita saba au hawapokei kabisa, je, ni lini Serikali itawaongeza mafuta hayo? Ahsante (*Makofi*)

SPIKA: Majibu kwa maswali hayo mazuri kutoka kwa Mbunge wa Bububu, Mheshimiwa Mwantakaje.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimponeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa ukaribu sana mazingira ya kazi ya askari wetu na kwa kweli watu wa Bububu hawakukosea na mimi mwenyewe nilishafika Bububu nikaona hali ya uhitaji wa usalama unavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, niseme tu katika muhula kwanza, katika mwaka wa fedha uliopita nusu mwaka ya kwanza ukilinganisha na nusu mwaka ya pili utaona kwamba bajeti ya mafuta iliongezeka. Katika bajeti tulioipitisha fedha ambazo tulitenga kwa ajili ya mafuta zilliongezeka. Nashukuru wenzetu wa Wizara ya Fedha wamekuwa wakizitoa fedha hizo ambazo zinaenda kwa ajili ya mafuta ili kuweze kuwezesha vijana wetu waweze kufanya doria kikamilifu. Kwa hiyo jambo hilo litafanyiwa kazi tunavyomiliza bajeti ili waweze kupata fedha hizo waweze kufanya doria kikamilifu. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda hauko upande wetu, naomba tumalizie hapo na tusikilizane kidogo.

Tumemaliza na swalii la Mheshimiwa Mwantakaje, Mbunge wa Bububu. Kule Bububu yeye ni Mbunge wa Jimbo aliwashinda CUF na wanamfahamu vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwantakaje na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid kutoka Mahonda kule hawa ni Wabunge wa Majimbo kutoka Zanzibar. Ukitaka habari zao waulizeni akina Mheshimiwa Masoud hapa wanawajua vizuri. (*Makofi/ Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nitambulisse wageni. Kwanza tunao wageni 13 ambao ni umoja wa wachezaji wa mpira wa miguu kutoka FC Grace kutoka nchini Marekani na wamekuja kwa ajili ya mchezo wa mpira miguu pamoja na Waheshimiwa Wabunge utakaofanyika kesho kutwa Jumamosi.

Our guests players from FC Grace from United State of America you are cordially welcome here at Dodoma and tomorrow you are going to have a soccer match with Bunge Sport Club, get prepared. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mchezo huo utachezwa saa 10 jioni, tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuhudhurie na mimi mwenyewe nitakuwa mgeni rasmi kwenye mchezo huo, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 31 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wachungaji kutoka Mkoa wa Dodoma. Wachungaji kutoka Mkoa wa Dodoma simameni pale mlipo. Ahsanteni sana na mtuombee, karibuni sana.

Baada ya wageni hao, kuna wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni walimu wawili na wanafunzi watatu kutoka Shule ya Wavulana ya Feza ambao walishinda medali ya dhahabu katika Mashindano ya Kimataifa ya Mazingira na Sayansi yaliyofanyika nchini Marekani. Wako wapi wale watoto wale wa *Feza Boys*? Wako upande gani?

Ooh kule! Naomba tuwapongeze sana kwa kushinda mashindano hayo huko Marekani, na wamepeperusha bendera ya Tanzania vizuri sana. (*Makofi*)

Sasa naomba niwatambulisse katika wale watatu, mmoja ni Abdallah Rubeya, nyoosha mkono, ahsante sana. Mwingine ni Kasi Juma Nkamia ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Juma Nkamia, kutoka Jimbo la Chemba hadi Marekani na kufanya mambo, kumbe hayo mambo yanawezekana. Lakini pia hongera kwa Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kwa sababu yupo Rashid Jakaya Kikwete. Ahsanteni sana, tunawapongeza sana, kila la heri na karibuni sana, karibuni sana watoto wetu.

Lakini pia wako walimu wao, Ndugu Ibrahim Yunus Rashid, Mkurugenzi na Ndugu Kadiri ambaye ni Mkuu wa Shule. Karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Baada ya hao niwatambulisse wageni ambaao ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mwigulu Nchemba, pale mlipo. Karibuni sana, karibuni wanangu. Hawa ni vijana ambaao ni watoto wa Mheshimiwa Nchemba, watoto wa kaka zake, wa dada zake, wa ndugu zake lakini pia ni watoto ambaao anawasomesha kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kwa taarifa nilizonazo ye ye binafsi huwa anawasomesha zaidi ya watoto 50. Kwa hiyo, hongereni sana wanangu, hongereni sana. (*Makofi*)

Kwa *spirit* hii ya Mheshimiwa Nchemba, siku moja mimi niliwahi kuhojiwa na mwandishi wa habari, akaniuliza una watoto wangapi? Nikamwambia hili swali ni gumu kweli kulijibu na wengi hawakunielewa kwa nini sikuweza kulijibu, ni kwa sababu hiyo. Mimi nina watoto wengi ambaao ni watoto wangu yaani wengi.

Sasa ukianza kusema watoto wale wa Kiingereza, Wakimarekani, Wakizungu sasa wale wengine utawaweka wapi na ni watoto wako? Kwa hiyo, nakupongeza sana, maana sisi Waafrika watoto ni *the larger family* siyo *the biological one*. (*Makofi/Kicheko*)

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Anastazia Wambura, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka *Dodoma Fitness Jogging Sports Club* wakiongozwa na ndugu John Israel Banda, wako pale karibuni sana wageni wetu wa *jogging*, karibuni sana. Siku moja mje mfanye *jogging* pale uwanja wa Jamhuri pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa *Bunge Sports Club* ili tuone; karibuni sana.

Tunao wageni 100 wa Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Singida ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mkoa wa Singida, UDOM-Singida. Ooh, karibuni sana wanafunzi wote kutoka Mkoa wa Singida, na Wabunge wenu wapo wanafanyakazi nzuri hapa Bungeni karibuni sana. Maendeleo makubwa hayo, Mkoa mmoja tu hebu angalia maneno haya halafu wakisimama jamaa zetu wanasema hakuna kilichofanyika, kweli jamani?

Wageni 27 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Mbozi Mkoa wa Songwe. Karibuni sana vijana 27 kutoka Mkoa wa Songwe kule Mbozi naamini siyo wote, hongereni sna lakini hiyo pia ni dalili njema. (*Makofi*)

Tunao wanafunzi 50 na walimu wanne kutoka shule ya sekondari ya *Peace House* ya Mkoani Arusha. Wale watoto kutoka Arusha, karibuni sana watoto wetu na walimu ambao mmefuatana nao. Maafisa wa Bunge watawapokea baadaye watawapa taarifa zote mnazozihitaji kuhusu Bunge, karibuni sana watoto wetu. (*Makofi*)

Tunao wanafunzi 70 na walimu sita kutoka shule ya Sekondari ya Kikuyu Mkoani Morogoro. Wanafunzi wa kutoka Morogoro! Nadhani bado wako njiani au wako *basement* mahali, wapo eehh? Wanafunzi wa Kikuyu kutoka Morogoro simameni. Karibuni sana, oooo! Mpo, karibuni sana wengine wako juu kule, karibuni sana watoto wetu. (*Makofi*)

Pia Kanisa la *Baptist Tanzania* lililoko Makole Mkoani Dodoma limeleta wageni wanane kutoka Uingereza ambao ni wachungaji na wageni hao wameambatana na wachungaji wenyeji. Wageni kutoka *Baptist Tanzania* na wageni wenu kutoka Uingereza, karibuni sana *Baptist Church.* (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kidogo, mtakumbuka maelezo ambayo niliyatoa jana kuhusu kazi ambazo zitaendelea kufanyika mara tu baada ya kipindi cha maswali ambapo tutaahirisha Bunge. Ni kwamba zile Kamati zetu zitaendelea. Kwa Kamati ya Mheshimiwa Doto Biteko ile yenye Kamati nne ndani yake ambayo pia Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa yenyewe itakutana ukumbi wa Msekwa *immediately* baada ya hapa. Kwa hiyo, nawaalika Wajumbe wa Kamati hizo nne kuhudhuria lakini pia Mbunge ye yote mwininge anayetaka kufika pale aweze kufika.

Nimemwambia Katibu wa Bunge aangalie habari ya mahudhurio halafu baadaye nitangalia, nitapima masuala yanayoendana na utaratibu. Kwa hiyo tunaombwa tuhudhurie kwa wingi kadri inavyowezekana. Na kwa hatua hii niseme shughuli zingine zozote, Kamati nyngine zozote zenye vikao vyovyyote vile vikao hivyo vimefutwa. Shughuli ni hii ambayo tumeisema inayoendelea hivi sasa, hiyo ni pamoja na Kamati ya Bajeti ambayo ilikuwa muende sijui wapi huko hakuna, shughuli ni hii ambayo iko mezani. Kwa hiyo, mnakaribishwa Msekwa. (*Makofii*)

Jioni kuanzia saa tisa kwa ule Muswada ambao unapelekwa kwenye Kamati ya Mheshimiwa Mchengerwa wao watakutana Utawala Annex kule kwenye zahanati mpya kwenye lile jengo la Mabenki Benki kule kuna ukumbi, kuanzia saa tisa kwa kamati ya Mchengerwa itakutana kule; lakini pia Wabunge mnakaribishwa pia wakati huo kuweza kushiriki katika shughuli hizo.

Watoto wa Mheshimiwa Lucy Magereli pale mlipo naomba msimame, wako pale, karibuni sana. (*Makofii*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge katika kumalizia naomba niseme maneno si mengi sana, tena niyaseme kwa upole maana watani zangu Wasukuma wanasema wakati mwingine unacharuka sana, sasa leo ngoja niwe mpole kidogo.

Katika uchangiaji wetu wa jana wako baadhi ya wenzetu ambao..., unajua sisi tunaokaa hapa mezani hatuchangii kama ninyi kazi yetu ni kuwapa nafasi nyinyi mseme, kwa hiyo, wakati mwingine zinzoka shutuma ambazo hatuna nafasi wala fursa ya kubishana na kulumbana, lakini wakati mwingine ni vizuri tukatumia fursa hizi kusafisha baadhi ya mambo au kuyaelezea baadhi ya mambo. Lakini sitagusa sana zilizo nyingi, nitagusa moja tu linalotokana na baadhi ya wenzetu ambao muda mwingi walikuwa hawapo lakini wakija wanachafua hali ya hewa halafu wanapotea.

Kwa hiyo, mwenzetu alisimama na *ku-claim* kwa nguvu nyingi kwamba Bunge hili ni dhaifu. Kwa maoni yangu hizi ndizo lugha za kuudhi, kwa sababu unapowaona wenzako wengi namna hii waliochaguliwa na watu, wakaletwa hapa halafu wewe unawaona *collectively* kwamba wao ni dhaifu, lazima *there is something wrong with you*. Huwezi tu hivi hivi unaakili timamu halafu ukawa unawaona wenzako wote ni kundi la wajinga fulani isipokuwa wewe una akili sana kuliko wao, unaotoa wapi maneno ya namna hiyo? (*Makof!*)

Yaani inafika mahali unashindwa hata kufikiri, yaani binadamu lazima uwe na staha ile ndogo tu ya kuwaheshimu binadamu wenzako hata kama hukubaliani nao katika mawazo. Watu wana familia zao, tuna watoto tunaleta hapa, tuna nchi inayotutegemea halafu mtu mmoja anasima anasema hawa watu dhaifu. Ni hawa hawa walisema Rais Jakaya Kikwete alipokuwa Rais dhaifu, hawa hawa. Niliwahi kusema wakati mwingine utawala mnaweza kuutengeneza wenyewe, mkauharibu wenyewe kwa midomo yenu. Kama mtu mtawala unamwambia dhaifu si anaamua kugangamala sasa kwamba twendeni,

aliyemfanya agangamale ni nani kama siyo wewe na mdomo wako? (*Makofi*)

Kwa hiyo, ndiyo maana saa hizi mnakimbia kimbia, mara sijui mnakwenda wapi, mara kufungua madudu gani huko sijui, hakuna cha kesi wala nini hapa mwaka mtu hakanyagi hapa. Mimi ndiyo Spika, narudia tena, mwaka mtu hakanyagi hapa, nenda wapi, nenda wapi mpaka tutaelewana kwamba hakuna udhaifu hapa. (*Makofi*)

Kuhusu huu Muswada ambao umeletwa, mimi kama Spika ninapopata Muswada wa namna hiyo au mwininge wowote ninauangalia kwanza kama mimi, lakini pili ninyi mmenichangulia watu wa kunishauri, wanaitwa Kamati ya Uongozi. Wajibu wangu mimi siyo kukataa mambo tu juu kwa juu, nikiliona kweli halifai kabisa nalikataa, lakini nikiliona lina mantiki fulani nalipeleka kwa wenzangu wanaitwa Kamati ya Uongozi, na Kamati ya uongozi mmechagua ninyi hawakuteuliwa na mtu yeoyote. Wale wanashauri baada ya hapo tunakubaliana kama jambo ni jema tunalileta kwenu kuptitia Kamati zenu ndiyo Kanuni zinavyotaka. Kamati zina mamlaka ya kuweza vile vile kumshauri Spika na kuishauri Kamati ya Uongozi kwamba jambo hili halijaiva, jambo hili hivi na tunataarifiana, ndiyo taratibu zetu. Siyo tunaposhughulikia jambo sasa tuitwe dhaifu kwa maana hiyo.

Kwa mfano, hili lililokuja ambalo tutakwenda tulishughulikie wote tuliangalie na tuone tunafanyaje. Pamoja na mambo mengine linaboresha ushiriki na umiliki wa Watanzania katika masuala ya madini, kwa kuanza kuwa na hisa asilimia 16 kuendelea hadi asilimia 50 kama tunavyolia siku zote Botswana wamekuwa na nchi nyngine. Hivi likija wazo la namna hiyo, la kuongeza *greep* ya Watanznaia katika umiliki wa rasilimali zao za asili walizopewa na Mungu mimi Spika nilikatae? Kwamba kwa ufanya hivyop litakuwa ni Bunge shujaa? Huo ndio ushujaa? (*Makofi*)

Linakuja jambo ambalo madini yasiyochenjuliwa hayatasafirishwa tena nje ya nchi. Mimi nilirudishie huko huko?

Kama yatasafirishwa basi watalipa VAT hapa hapa nchini nilizuilie huko huko? (*Makofi*)

Linakuja jambo ambalo tunajua linapunguza *discretionary powers* za Waziri na Kamishina wa Madini ambazo ziliikuwa zinaleta shida siku za nyuma kwa uzoefu wetu, sasa tunazipunguza, si ndiyo jambo tulikuwa tunalipigia kelele fulani kafanya hivi, fulani kafanya hivi, tulizuilie huko huko? Sasa watakuwepo Makamishina watatu watakaoamua kwa pamoja na baada ya maamuzi yao ya mikataba italetwa kwenye Baraza la Mawaziri na badaa ya hapo italetwa katika Bunge, Bunge linapata *veto powers* ya kuangalia hayo mambo, wewe ungekuwa Spika unaletewa pendekemo la namna hii unalirudishia huko huko? Eti ndiyo unaonekana Spika mahiri, Spika makini? Na faida nyingine nyingi sitaki kuuchmabua huu Muswada. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ndugu zangu pamoja na yote ninachojaribu kusema ni nini? ni kuwa tu na heshima kwa mawazo ya watu wengine. Hata hao wenzetu hao tunaokimbilia Majaji, kuna mahali linakaa benchi la Majaji watatu. Majaji wawili wanaweza wakaamua jambo, mmoja akaamua tofauti, wakishapiga kura yule mmoja inaingia katika *record* kama ni *descending opinion* ya yule mmoja, *descending opinion*. Hasimami tu kusema wale wengine wale wapumbavu wale, wale hawakusoma hawaelewi wale, hapana.

Ni mawazo yake, yametofautiana na yale ya waliowengi na anaheshimu mawazo ya wale wengine na ye ye hata ukimuuliza kwanini wenzako waliamua kitu fulani? Atasema wale wliamua tofauti kwa sababu mtazamo wao wao ni sababu yake hii na hii, tukienda hivyo tutakwenda vizuri tu, ukiwaelewa wanatofautiana na wewe na ukajua na sababu zao. Hata hivyo utazielewa kama wanaku heshimu, lakini kama mtu hakuheshimu, anakusemea mbovu, hivi utamsikiliza? kwanini umsikilize? Haiwezekani!

Kwa hiyo, ndugu zangu katika Bunge letu kinacholeta matatizo humu ndani ni tabia na lugha, tukirekebisha hayo mawili, tabia na lugha za humu ndani tutakwenda vizuri tu.

Lakini najua kundi hili ni kubwa kwa hiyo hili tutaendelea kulisema lakini pale ambapo ni lazima tutachukua hatua. (*Makofî*)

Baada ya maelezo hayo sasa ndugu zangu, miongozo yote tunaiahirisha, ni kazi tu tunakwenda kule ambako tumeelekezwa kwa wale wenyefursa ya kufanya hivyo, lakini wale Wajumbe wa Kamati niwaombe sana tuhudhurie ndiyo maana tumeweka Kamati nydingi kwa wakati mmoja kwasababu hatuna cha kuficha chochote kile. Na kwa sababu hatuna cha kuficha ndiyo maana tunesema Wabunge wote mnakaribishwa kwenye jambo hilo kule na baadae tutakuja kulishughulikia jambo hilo hapa.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa nichukue fursa hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu saa 3:00 asubuhi na shughuli hizo zitaendelea na kesho na Jumapili tukumbuke kwenye Kamati. Ahsante sana.

(Saa 4.38 Asubuhi Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 3 Julai, 2017, Saa Tatu Asubuhi)